

Kwa nini Allah ataadhibu kwa moto?

Atakayejitenga na mama yake na baba yake akawadhilisha akawafukuza kutoka kwenye nyumba wakawa wanatanga barabarani ni ipi hisia zetu kwa huyu mtu?

Mtu mmoja akasema ataishi nayo katika nyumba yake atamkirimu, atamlisha atamshukuru kwa kazi hii, hivi watu watamkubalia kwa kitendo hicho? Allah yupo mbali na kupigiwa mfano, Tunatarajia nini yawe mafikio ya yule aliyemkataa na kumpinga (kufuru) Muumba wake? atakaye adhibiwa kwa moto ni kama amewekwa sehemu yake sahihi. Huyu mtu dharau amani na heri ardhini kwa hiyo hastahiki kupata neema peponi.

Tunatarajia lipi kwa yule anaye waadhibu watoto kwa mfano na silaha za kemikali aingizwe peponi bila kuhesabiwa?

Dhambi zao hazina mpaka wa muda bali tabia isiyoondoka.

Na kama wangeli rudishwa bila ya shaka wange yarejea yale yale waliyo katazwa. Na hakika hao ni waongo. 28

Wao wanamuelekea Allah kwa kiapo na uongo, na wao watakuwa mbele ya Allah Siku ya kياما.

Siku atakayo wafufua Mwenyezi Mungu wote, wamuwapie kama wanavyo kuwapieni nyinyi. Na watadhani kuwa wamepata kitu! Kwa hakika hao ndio waongo. 18

Kama shari ilivyo huwa inatokea kwa watu kutoka katika nyoyo zao kwa hasadi, wivu na husababisha kueneza matatizo na ugomvi kati ya viumbe. Ikiwa katika uadilifu iwe malipo yao ni moto na ndio inayoendana na tabia yao.

Na wale watakao kanusha Ishara zetu na wakazifanyia kiburi, hao ni watu wa Motoni; humo watadumu.36

Sifa ya Allah ni mwadilifu inajulisha kuwa yeye anaadhibu kwa Rehema zake. Allah kwa mujibu wa imani ya wakristo ana mapenzi tu. Kwa upande wa wayahudi wanaamini Allah ana hasira tu. Katika uislamu Allah ni muadilifu

mpole ana majina mazuri yote, nazo ni sifa za uzuri na utukufu.

Kisha katika uhalisia kimatendo katika maisha tunatumia moto kuondoa uchafu kutoka kwenye kitu kisafi mfano katika dhahabu na fedha. Kwa sababu hiyo Allah (Allah yupo mbali nakupigiwa mfano) hutumia moto kuwasafisha wajawake akhera kutokana na madhambi na maovu. Muislamu atatoka motoni mwishoni kabisa yule ambaye alikuwa ana imani mfano wa uzito wa sisimizi kwa huruma yake.

سؤال وجواب حول الإسلام

Source: <https://www.nwahy.com/qa-islam/sw/120/>

Arabic Source: <https://www.nwahy.com/qa-islam/ar/120/>

Sunday 3rd of May 2026 08:08:17 PM